**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027


**Dkt. JUMA MALIK AKIL (MBM),**
**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**


**JUNI,2026**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** niendeleze shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwanza kwa kuniteua kua mjumbe wa Baraza hili tukufu na kuniteua kua Waziri mwenye dhamana ya kuisimamia sekta ya Fedha na Mipango ili niweze kumsaidia kutekeleza majukumu yake, hususan katika kusimamia fedha za umma na uchumi kwa ujumla. Kwa imani hii, nimuhakikishie kua majukumu haya nitayasimamia vyema kwa kadiri ya uwezo wangu hususan katika maeneo ya ukusanyaji, utafutaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwenye miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii ili kuchochea maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

3. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru, **Mheshimiwa Hemed Suleiman** Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa hekima, ufanisi na kazi nzuri anayoifanya ya kushauri, kusimamia utendaji wa Serikali na kuwatumikia wananchi. Tunamshukuru kwa usimamizi na tutaendelea kupokea maelekezo yake katika kutimiza majukumu tulipewa kikatiba kwa maslahi na mustakabali wa taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid**, Spika wa Baraza la Wawakilishi

na **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma**, Naibu Spika kwa kuliongoza Baraza kwa umahiri mkubwa kwa kushirikiana na Wenyeviti wa Baraza.

5. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kutoa shukrani zangu za kipekee kwa Kamati ya Kudumu ya Bajeti inayoongozwa na **Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir** kwa ushirikiano wao katika kuhakikisha tunatimiza azma ya Serikali ya kuwahudumia wananchi. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/27. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kufikia bajeti hii ninayoiwasilisha leo.

6. **Mheshimiwa Spika**, pia, nawapongeza waheshimiwa wawakilishi wote, wale ambao wamepata nafasi ya kurudi tena barazani na wawakilishi wapya walioingia barazani baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliofanyika Oktoba 29 mwaka 2025 ambapo ulifanyika kwa amani na mafanikio makubwa.

7. **Mheshimiwa Spika,** mbali ya shukrani hizo za awali naomba pia kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati wasaidizi wangu wakuu wakiongozwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa **Dkt. Hamad Omar Bakari**, Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni, Kaimu Katibu Mkuu **Ndugu Aboud Hassan Mwinyi**, na Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango **Dkt. Afua Khalfan Mohamed** kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo. Pia, ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi za taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, Uongozi wa Wizara, wakuu wa taasisi na watumishi wote kwa ushirikiano na kujituma katika kutekeleza majukumu yao.

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kutumia fursa hii kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango yenye sehemu kuu nne (4) kama ifuatavyo:- Utangulizi, Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Vipaumbele na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na Viambatisho vya taarifa za fedha za Mapato na Matumizi.

## B. MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

9. **Mheshimiwa Spika,** Kimuundo Wizara ya Fedha na Mipango (iliyokuwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango) imejumuisha mafungu makuu (7) ambayo ni Wizara ya Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango (F03), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali (F06) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (F07). Vile vile Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia Taasisi Nane (8) zinazojitegemea ambazo ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar (TRA), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA), Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi (ZIAAT) na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF).

## C. MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango imepangiwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

a) Kusimamia mapato ya Serikali kutokana na vyanzo mbali mbali

yanayojumuisha mapato ya kodi na yasiokuwa ya kodi, misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

b) Kusimamia mali za Serikali kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali katika Mashirika na Kampuni binafsi ambazo Serikali inamiliki;

c) Kusimamia Fedha za Umma, shughuli za Uhasibu na Ukaguzi Serikalini. Katika jukumu hili Wizara inasimamia Bajeti ya Serikali, usimamizi wa Hazina, huduma za Uhasibu na Ukaguzi wa ndani Serikalini;

d) Kusimamia Deni la Taifa kwa kutoa ushauri, kufuatilia mwenendo wa Deni la Taifa (Mikopo ya Ndani na Nje) na udhibiti wake;

e) Wizara inasimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha, inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na usimamizi wa Taasisi za huduma ndogo za fedha;

f) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;

g) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi kupitia sekta za kiuchumi na kijamii;

h) Kuratibu sera za kitaifa na kisekta za kupunguza umaskini nchini;

i) Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi; na

j) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya kitaifa na kimataifa.

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI HADI KUFIKIA MACHI 2026 MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Mapato

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kukusanya **TZS 6,527.599 bilioni**

kupitia mafungu yake ya F01, F04, F05 na F07. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, Wizara ilikadiria kukusanya **TZS 4,351.313 bilioni** ambapo, hadi kufikia mwezi Machi 2026 **TZS 3,217.341 bilioni** zilikusanywa, sawa na asilimia **74** ya makadirio ya kipindi cha tathmini.

12. **Mheshimiwa Spika,** kutofikiwa kwa asilimia 100 ya lengo la ukusanyaji mapato kunatokana na sababu mbali mbali zikiwemo upatikanaji mdogo wa fedha za mikopo kwa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Wizara imefanikiwa kukusanya zaidi katika mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo **TZS 2,046.780 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia **36** zilikusanywa katika kipindi kama hicho. Sababu za mapato hayo kuongezeka ni kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi, kuboresha mazingira bora ya uwekezaji na uwajibikaji. Mchanganuo wa Mapato hayo kwa mafungu ni kama ifuatavyo: -

**Mapato Fungu F01 (Wizara ya Fedha na Mipango)**

13. **Mheshimiwa Spika,** Fungu F01 katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kukusanya **TZS 3,518.629 bilioni**. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, Fungu F01 lilikadiriwa kukusanya **TZS 2,085.511** bilioni, hadi kufikia Machi **TZS 2,013.861 bilioni** zimekusanywa, sawa na asilimia **97** ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yamejumuisha mapato ya kodi, mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mapato mengineyo.

**Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F04 limekadiriwa kukusanya **TZS 0.180 bilioni**. Katika kipindi cha Julai -

Machi 2026, Ofisi imekadiriwa kukusanya **TZS 0.130 bilioni** ambapo, hadi kufikia mwezi Machi 2026 **TZS 0.061 bilioni** zilikusanywa sawa na asilimia **47** ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yamekusanywa kupitia vyanzo vyake vya utoaji wa Vibali vya utafiti na Ukodishwaji wa kumbi za mikutano. Upungufu wa ukusanyaji wa mapato umesababishwa na kufanya marekebisho ya matumizi ya kumbi za mikutano na kuwa ofisi zinazotumika na wafanyakazi. Aidha, katika kipindi hicho ofisi haikuweza kukusanya mapato ya uuzaji wa vitabu (ushauri elekezi).

**Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)**

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F05 limekadiriwa kukusanya **TZS 2,980.289 bilioni**. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2026, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imekadiriwa kukusanya **TZS 2,240.411 bilioni** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2026, **TZS 1,187.315 bilioni** zilikusanywa sawa na asilimia **53** ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Mapato haya yamekusanywa kupitia Mapato ya Wafanyakazi (PAYE), Mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Misaada ya Kibajeti (GBS), Hati fungani, Gawio la Benki Kuu na Mapato mengineyo.

**Fungu F07 (Ofisi ya Msajili wa Hazina)**

16. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu F07 limekadiriwa kukusanya **TZS 28.5 bilioni**. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026 Ofisi imekadiriwa kukusanya **TZS 25.26 bilioni** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2026, **TZS 16.104 bilioni** zilikusanywa, sawa na asilimia **64** ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yamekusanywa kupitia Gawio la Mashirika, Kodi ya Bohari, Uuzaji wa vifaa vikongwe, Kodi za majengo ya serikali yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango na Mapato ya Mashamba. Kutokana na

kuhamishwa kwa baadhi ya rasilimali za Serikali kutoka Wizara ya Fedha, mapato ya ofisi hiyo pia yalipungua.

Mchanganuo wa Mapato kwa ujumla yanaonekana katika **kiambatanisho namba 1**.

**Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango.**

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Fedha na Mipango ilipangiwa kutumia **TZS 1,571.151 bilioni.** Kwa kipindi cha Julai - Machi 2026, Wizara imepangiwa kutumia **TZS 1,280.912** bilioni na hadi kufikia Machi 2026 **TZS 1,154.017 bilioni** zimetumika, sawa na asilimia **90** ya makadirio ya katika kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya mishahara **TZS 23.922 bilioni;**
ii. Matumizi ya uendeshaji wa mafungu ya Wizara ya Fedha **TZS 585.395 bilioni**;
iii. Ruzuku zilizopatiwa Taasisi za Wizara **TZS 26.719 bilioni;** na
iv. Matumizi ya miradi ya maendeleo **TZS 517.981 bilioni**.

18. **Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa mafungu yaliyopo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ni kama ifuatavyo: -

**Fungu F01 (Wizara ya Fedha na Mipango)**

19. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F01 yamejumuisha programu kuu tatu (3) ndani yake zinajumuisha programu ndogo nane (8), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 fungu limepangiwa kutumia **TZS 866.134 billioni**. Hadi kufikia Machi 2026, Fungu hili limetumia **TZS 549.679 bilioni** sawa na asilimia **88** ya makadirio

ya **TZS 622.475 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa fedha hizo kwa Programu ni kama ifuatavyo: -

## PF0101-Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma

**20. Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali, hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 27.257 bilioni** sawa na asilimia **66** ya makadirio ya **TZS 41.230 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali, Programu ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje na Programu ndogo ya Kusimamia Sera za Kodi na Fedha na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Kutoa uelewa juu ya masuala ya uimarishaji wa taarifa zinazohusika na maandalizi ya Bajeti inayozingatia matokeo (Program Based Budget) kwa lengo la kuwezesha maafisa kutayarisha bajeti kwa kuzingatia matokeo;

ii. Kuandaa Hotuba ya Bajeti toleo la wananchi (citizen budget) kwa lugha nyepesi na picha ili kuwawezesha wananchi wote kuelewa mipango na malengo ya Serikali kwa urahisi;

iii. Kutoa mafunzo ya kuandaa mpango wa matumizi (Cash Flow) kwa MDAs & LGAs Unguja na Pemba ili kuziwezesha sekta kupanga kulingana na mahitaji na muda sahihi kwa kuzingatia Matakwa ya Serikali;

iv. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 (Budget Monitoring and Accountability) kwa Wizara nane kwa lengo la kuimarisha upangaji na utekelezaji mzuri wa Bajeti ya Serikali;

v. Kushiriki kikao cha kujadili mgawanyo wa fedha za mradi wa Kuboresha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (SCALE) na

namna bora ya utekelezaji wa mradi huo, ambapo jumla ya dola za Kimarekani 11,800,000 zitapokelewa kutekeleza kazi za mradi huo;

vi. Kushiriki vikao vya kitaalamu vya majadiliano ya mikopo na washirika wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo Submarine Cable Power Supply kutoka AfDB na Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program for result PHASE II kutoka Benki ya Dunia;

vii. Kushiriki kikao cha makabidhiano ya ujenzi wa uwanja wa ndege kisiwani Pemba kwa mkandarasi PROPAV ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuimarisha uchumi wa Zanzibar kwa kuufanyia maboresho uwanja huo ili kuweza kutanua huduma za usafirishaji kisiwani humo;

viii. Kusimamia utoaji wa misamaha ya kodi ambapo jumla ya misamaha 474 ilipokelewa kati ya misamaha hiyo jumla ya misamaha 367 ilikubaliwa, iliyokataliwa ni 65 na misamaha 42 ilishindwa kukidhi vigezo vya uombaji wa misamaha; na

ix. Kufanya mapitio ya ada na tozo zilizowasilishwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili zinazotozwa katika maeneo ya hifadhi za misitu Zanzibar, hatua iliyosaidia kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu.

**PF0102-Programu Kuu ya Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Sheria**

21. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuandaa na kusimamia Sera za Ununuzi pamoja na kuandaa mazingira bora ya kazi katika masuala ya kisheria. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 2.348 bilioni** sawa na asilimia **72** ya makadirio ya **TZS 3.282 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha programu

ndogo mbili (2) ambazo ni programu ndogo ya Usimamizi wa Sera za Ununuzi na programu ndogo ya Huduma za kisheria za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo:

i. Kukamilisha rasimu ya awali ya Kanuni za Maadili ya Ununuzi wa Umma kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 123 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma;
ii. Kupitia upya muundo wa kada ya ununuzi na kuunda kamati maalum ya tathmini ambapo ripoti ya muundo huo imekamilika;
iii. Kuandaa rasimu ya sheria ya uanzishwaji upya wa Chuo cha Fedha ambayo inaendelea na taratibu za kiserikali kabla ya kuanza utekelezaji wake; na
iv. Kuratibu vikao vya bodi ya rufaa za kodi, jumla ya mashauri 91 yamefunguliwa kati ya mashauri hayo, 87 yanaendelea kusikilizwa na mashauri 4 yamekamilika na kupelekea Serikali kuokoa kiasi cha USD 104,231.06 na TZS 5,488,882.37 zilizowasilishwa Serikalini.

**PF0104– Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango**

22. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uendeshaji wa shughuli za sekta ya fedha. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 520.074 bilioni** sawa na asilimia **90** ya makadirio ya **TZS 577.692** bilioni kwa kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha programu ndogo ya Uendeshaji na Utumishi, program ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha na programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba na kutekeleza shughuli kadhaa zikiwemo:

i. Kusimamia na kuwapatia haki zao wafanyakazi ambapo wafanyakazi 55 wamepatiwa likizo zao za kawaida kati ya hao wafanyakazi 12 walipatiwa stahiki zao za malipo ya nauli ya likizo;

ii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa kufanya ununuzi wa vifaa mbalimbali ikiwemo vya kuandikia, kompyuta na mashine za kurudufu pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi kwa upande wa Unguja na Pemba;
iii. Kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi 24 wanaoendelea na mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 14 wa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ikiwemo sekta ya fedha, Sheria za kazi na masuala mtambuka. Hatua hii imechangia kuimarika kwa ujuzi, weledi na ufanisi wa watumishi katika utekelezaji wa majukumu yao;
iv. Kuratibu na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na kuratibu shughuli za Baraza la Wawakilishi hatua iliyochangia kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu na kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za kiserikali;
v. Kupitia Maafisa Takwimu, ofisi imefanikiwa kuchakata takwimu za fedha za Serikali pamoja na madeni ya Serikali kwa miaka ya fedha 2023/2024 na 2024/2025, kwa kushirikiana na wataalamu kutoka IMF na EAC, ili kuboresha ubora wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa hizo;
vi. Kuratibu na kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti 2024/2025, ripoti za robo ya kwanza na ya pili kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo imeonesha hali halisi ya kiwango cha utekelezaji wa bajeti na matumizi ya rasilimali katika wizara ili iweze kusaidia katika upangaji wa bajeti zinazofuata;
vii. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati hatua itakayowezesha kuimarika kwa upangaji na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na kufikiwa kwa malengo ya maendeleo kwa ufanisi zaidi; na

viii. Wizara ya Fedha na Mipango - Ofisi Kuu Pemba ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara 18 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 4 kwa ajili ya kuboresha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

**Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)**

**PF0201 Program Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali**

23. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F02 limepangiwa kutumia **TZS 641.350 bilioni**. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, fungu limetumia **TZS 561.070 bilioni**, sawa na asilimia **92** ya makadirio ya **TZS 608.725 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuhudumia Mfuko wa Madeni;
ii. Kulipa Pencheni Jamii kwa wastani wa wazee **33,364** waliofikia miaka 70;
iii. Kulipa Pencheni kwa wastani wa wastaafu **13,426** wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
iv. Kulipa mafao ya Kiinua Mgongo kwa wastaafu **811** wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
v. Kulipa Mishahara ya Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na
vi. Kulipia matumizi mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar)**

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Mipango imepangiwa kutumia **TZS 20.380 bilioni**. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, Tume ilitumia **TZS 16.513 bilioni** sawa na asilimia **93** ya makadirio ya **TZS 17.848 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: -

**PF0301-Programu Kuu ya Uratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi**

**25. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa mipango hiyo. Programu hii ina jumla ya Programu ndogo tatu (3), ambazo ni program ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini; program ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu na program ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 13.993 bilioni** sawa na asilimia **106** ya makadirio ya **TZS 13.258 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Uhakiki wa programu na miradi ya maendeleo Unguja na Pemba kwa lengo la kupata taarifa za utekelezaji na kukamilisha taratibu za maombi ya fedha, ambapo jumla ya programu 31 na miradi 47 ilihakikiwa. Programu na miradi iliyohakikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za maendeleo, uimarishaji wa miundombinu ya elimu na afya, ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa hospitali, barabara za ndani, ujenzi wa ofisi za Masheha, miradi ya mifugo na misitu, bandari ya Mangapwani, Mahanga na nyumba za askari na masoko ya kisasa ya samaki;

ii. Kuhakiki na kupitisha Miradi sita (6) ya maendeleo iliyowasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo kutafutiwa fedha. Miongoni mwa miradi hiyo ni Ujenzi wa Kituo Kidogo cha Umeme cha 132/33 KV Dunga na 'Upgrading Unguja's Submarine Powers Supply Kutoka 45 MW to 100 MW kwa ajili ya kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa nishati ya Umeme;

iii. Kuandaa na kuwasilisha kwa wadau Muongozo wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo Kazini (Zanzibar Internship Guideline). Muongozo

huo utawezesha wahitimu wa vyuo mbalimbali kupata uzoefu wa kazi kabla ya kuingia katika soko la ajira, sambamba na hatua za awali za kuunganisha mfumo wa wahitimu (Rasilimali Watu) na mfumo wa Utumishi wa Umma ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi;

iv. Kuanda na kuzindua Ripoti kuhusu Masuala ya idadi ya watu na mabadiliko ya tabia nchi ambapo jumla ya nakala 170 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbali mbali. Ripoti hizi zinasaidia kutoa ushahidi juu ya kupanga mipango kwa kuzingatia idadi ya watu na mabadiliko ya tabia nchi;

v. Kuandaa rasimu ya ripoti ya awali ya kutathmini utayari wa nguvu kazi ya Zanzibar ili kukidhi matarajio ya kimkakati ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 (Zanzibar National Skills Development toward attaining ZDV 2050 Aspirations). Aidha Rasimu ya Awali ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Nguvu kazi ya Taifa (Human Capital Development Strategic Plan) imeandaliwa; na

vi. Kuandaa ripoti ya programu na miradi ya maendeleo 60 kati ya 97 sawa na asilimia 61.9, Ripoti hiyo imeonesha hatua za utekelezaji, changamoto na mapendekezo ya utatuzi wa changamoto hizo.

**PF0302-Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Tafiti**

26. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia Sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa vya Tafiti zitakazosaidia ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu. Programu hii ina jumla ya programu ndogo mbili (2) ambazo ni programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi na programu ndogo ya Uratibu wa Tafiti na Ubunifu. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 1.029 bilioni** sawa na asilimia **45** ya makadirio ya **TZS 2.266 bilion**i ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zikiwemo; -

i. Kuandaa ripoti tisa (9) za hali ya mfumuko wa bei na kuwasilishwa katika Kamati ya Ukomo (Ceiling Committee) pamoja na kutoa ripoti tatu (3) za mwenendo wa hali ya uchumi kwa robo mwaka;

ii. Kuratibu utoaji wa mafunzo kuhusu uchumi wa kidijitali kwa Wakurugenzi Mipango na maafisa kutoka sekta za Serikali na binafsi kwa Unguja na Pemba;

iii. Kutoa ripoti ya mwelekeo wa hali ya Uchumi (2026 _ 2028) kwa kutumia Financial Programming (FP) modeli na kusaidia katika miongozo mbali mbali ya Serikali ikiwemo utayarishaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027;

iv. Kujengea Uwezo watendaji 29 kutoka Taasisi za Serikali juu ya mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi taarifa za tafiti (ZARIP). Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuziwezesha taasisi kuingiza na kupokea taarifa za tafiti ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za tafiti na taarifa nyengine ziweze kutumika na kusaidia katika sera, miongozo na kufanya maamuzi;

v. Kuratibu kikao cha wadau wa usalama barabarani ili kuimarisha mikakati ya kupunguza ajali, kikihusisha taasisi mbalimbali zikiwemo Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Jeshi la Polisi (Kitengo cha Usalama Barabarani), Mabalozi wa Usalama Barabarani na Wakala wa Barabara; aidha, mabalozi 70 walipatiwa mafunzo ya mbinu bora za kusimamia usalama barabarani ili kupunguza ajali zinazosababisha upotevu wa maisha na mali; na

vi. Kufanya vikao vya kusambaza matokeo ya tafiti zinazohusu masuala ya Afya kwa upande wa malaria, matumizi endelevu ya Maji kwa ajili ya umwagiliaji na Ajira kwa vijana, vimefanyika na kushirikisha jumla ya washiriki 65 Unguja na Pemba (Unguja 35 na Pemba 30), kwa lengo la usambazaji wa matokeo na kuwezesha wadau kutumia matokeo ya tafiti pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika muhtasari wa sera (Policy Briefs).

**PF0303-Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango**

27. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Programu hii ina jumla ya programu ndogo mbili (2) ambazo ni program ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango Pemba. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 1.490 bilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya **TZS 2.323 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zikiwemo: -

i. Kusimamia upatikanaji wa huduma za kiuendeshaji kwa Tume ya Mipango Unguja na Pemba ili kuimarisha utendaji kazi Pamoja na kuwapatia stahiki za wafanyakazi ikiwemo nauli za likizo kwa wafanyakazi 12;

ii. Kufanya mapitio ya Mkataba ya Utoaji huduma kwa umma kwa lengo la kubainisha huduma na kuweka ahadi juu ya utoaji wa huduma kwa wadau Pamoja na kufanya mapitio ya Mpango Mkakati hatua itakayowezesha kuimarika kwa upangaji na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi;

iii. Kuratibu upatikanaji wa Mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watano (5), katika fani za Mipango na Maendeleo ya jamii, TEHAMA na Sheria. Vile vile, mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi watano (5) katika fani ya udereva, Katibu Muhtasi na mafunzo ya kujiandaa na kustaafu. Vile vile mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 55 wa Tume ya Mipango kuhusiana na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao katika masula ya sheria, kanuni na miongozo ya kazi yametolewa; na

iv. Kuratibu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Tume ya Mipango zinazofanyika kupitia Ofisi ya Uratibu - Pemba pamoja na

kushiriki vikao kazi kwa viongozi na maofisa wa Ofisi ya Uratibu vinavyofanyika Unguja.

**Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F04 limepangiwa kutumia **TZS 11.607 bilion**i. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, Ofisi imetumia **TZS 7.894 bilioni** sawa na asilimia **105** ya makadirio ya **TZS 7.523 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo: -

**PF0401-Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii**

29. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuongeza ubora na wingi wa takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Programu hii hadi Machi 2026, imetumia **TZS 4.691 bilion**i sawa na asilimia **100** ya makadirio ya **TZS 4.709 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii kuu imejumuisha programu ndogo mbili (2) ambazo ni Programu ndogo ya Ukusanyaji, Uchambuzi na Uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii na programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Kitakwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar. Programu hii imetekeleza shughuli zikiwemo:-

i. Kukusanya, kuchakata na kutoa jumla ya ripoti 36 za kitakwimu za kila mwezi na robo mwaka na kusambaza kwa wadau kwa njia ya tovuti, machapisho na vyombo vya habari. Ripoti hizo zinajumuisha mfumuko wa bei, Utalii, Ajali barabarani na Udhalilishaji wa kijinsia baadhi ya ripoti hizo kama ifuatavyo:

a. Ripoti ya mfumko wa bei inaonesha kupungua kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2025, ambapo ulipungua kutoka asilimia 4.05 Julai 2025 hadi 3.47 Septemba 2025. Aidha, katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025, mfumko wa bei uliendelea kushuka hadi asilimia 3.34 Novemba 2025, kabla ya kupanda kidogo na kufikia asilimia 3.81 Desemba 2025. Hata hivyo, kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2026, mfumko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 4.25 Januari 2026 hadi kufikia asilimia 4.93 Machi 2026; na

b. Ripoti ya takwimu za Utalii inaonesha jumla ya watalii **800,968** waliwasili nchini kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, sawa na ongezeko la Asilimia **21.9** ukilinganisha na Watalii 656,194 walioingia Kipindi kama hichi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Watalii wengi waliwasili kutoka nchi za Italia, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, Poland na Marekani.

ii. Kwa kushirikiana na Wizara ya Takwimu ya Korea, ofisi imefanya ufunguzi wa mfumo wa kutoa Taarifa za Kitakwimu (ZANSIS) pamoja na marekebisho ya chumba cha kuhifadhia taarifa. Aidha, kwa sasa ofisi inaendelea kutoa mafunzo ya namna ya kuutumia na kuuendeleza mfumo huo ili kuweza kuisaidia utoaji wa taarifa kwa Mtumiaji kwa wakati;

iii. kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ofisi imekamilisha kuratibu Daftari la Sensa la shughuli za Kiuchumi na Kijamii kwa kuingiza taarifa za Taasisi mbali mbali zikiwemo Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), BPRA na TRA. Aidha, Ofisi imeshakamilisha kanzidata ya Daftari hilo na tayari ipo katika tovuti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na NBS;

iv. Ofisi inasimamia shughuli za tafiti kupitia maombi ya vibali kwa kipindi cha Julai 2025 - Machi 2026, ambapo jumla ya vibali 981 vimetolewa kati ya hivyo 868 vilitolewa kwa wanafunzi, 55 vimetolewa kwa Taasisi, vibali tisa 9 vimetolewa kwa watafiti binafsi na vibali 49 kwa wageni; na
v. Ofisi imekamilisha uhakiki wa utafiti wa nguvu kazi (ILFS) kwa mwaka 2025 kwa ajili ya kuunganisha taarifa na Tanzania Bara ili kuandaa ripoti kuu ya Tanzania kwa ujumla.

**PF0402-Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

**30. Mheshimiwa Spika,** Programu hii hadi Machi 2026, imetumia **TZS 3.202 bilioni** sawa asilimia **114** ya makadirio ya **TZS 2.814 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha programu ndogo mbili (2) ambazo ni program ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja; na Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba. Program hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wanane (8) na kupatiwa nyongeza zao kwa mujibu wa sheria. Aidha, Ofisi inaendelea na zoezi la kufanya uhakiki wa taarifa za wafanyakazi kupitia mfumo wa HRP na baadhi ya changamoto zilizojitokeza zimeanza kufanyiwa kazi ikiwemo ujazaji wa taarifa za wafanyakazi kwenye mfumo pamoja na kunakili taarifa za watumishi na kuingizwa kwenye mfumo;
ii. Kusimamia stahiki za watumishi kupitia mpango wa likizo wa mwaka 2025/2026 jumla ya Watumishi 28 wamepatiwa likizo, kati ya hao watumishi 14 wamepatiwa posho la Likizo kwa mujibu wa sheria na mtumishi mmoja (1) amepatiwa likizo ya dharura;

iii. Jumla ya Watumishi watano (5) wameruhusiwa kwenda masomoni katika vyuo mbali mbali ili Kuwajengea uwezo wa kitaaluma ; na

iv. Matumizi ya uendeshaji wa Ofisi yamefanyika kupitia huduma mbali mbali zikijumuisha upatikanaji wa huduma ya maji, usafi, umeme, mafuta na mawasiliano pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuandikia na Samani za Ofisi katika kipindi cha utekelezaji.

**Fungu F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.**

31. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F05 limepangiwa kutumia **TZS 17.589 bilioni.** Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, fungu hili limetumia **TZS 10.532 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 13.444 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo:-

**PF0501 – Programu kuu ya Usimamizi wa Hazina**

32. **Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina lengo la kusimamia fedha za umma pamoja na kufanya usuluhishi wa hesabu za mapato kwa Serikali. Progamu hii imejumuisha programu ndogo nne (4) ambao ni Programu ndogo ya Ufuatilaiji wa Mapato ya Serikali Yasiyokuwa ya Kodi, programu ndogo ya Kusimamia Ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali, programu ndogo ya Usimamizi wa Matumizi ya Serikali na programu ndogo ya Usimamizi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu. Hadi kufika Machi, 2026 programu imetumia **TZS 0.880 bilioni** sawa na asilimia **39** ya makadirio ya **TZS 2.266 bilioni** katika kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zikiwemo: -

i. Kuandaa Rasimu ya miongozo ya kuhamia matumizi ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha (IPSAS Accrual) pamoja na matumizi ya mfumo wa BAMAS kwa taasisi zisizo za kibajeti;

ii. Kushiriki katika vikao kazi vya maboresho ya mfumo wa BAMAS kwa lengo la kuboresha uwezo wa mfumo katika kuandaa na kutoa taarifa za fedha kwa taasisi za umma;
iii. Kuratibu vikao tisa vya kamati ya ukomo wa mapato na matumizi (Ceiling Committee meeting) na kutoa mgao wa fedha kwa Wizara na taasisi za Serikali kila mwezi ili kuziwesha taasisi hizo kuweza kutekeza majukumu waliyojipangia;
iv. Wafanyakazi watano walishiriki ziara ya kikazi Dodoma kwa kushirikiana na watendaji wa Hazina Bara katika kuboresha mfumo na kuandaa ripoti za mwisho wa mwaka. Aidha, wafanyakazi watatu walifanya ziara ya kikazi kujifunza utaratibu wa malipo ya mishahara na usimamizi wa mikato, kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa mifumo ya malipo;
v. Kushiriki katika kikao kazi cha kuboresha moduli ya ununuzi (Purchase Module) umefanyika, ambapo ujuzi juu ya uingizaji wa taarifa za awali (Opening Balance) na marekebisho ya hesabu za mwisho wa mwaka umeimarishwa;
vi. Vikao vinne (4) vya kawaida vya Kamati ya Kitaalamu ya Usimamizi wa Deni la Taifa, vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa, vimeratibiwa. Vikao hivyo vimechangia kufanikisha upatikanaji wa dhamana katika taasisi za Serikali;
vii. Jumla ya wafanyakazi 308 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali wamewezeshwa kupatiwa mikopo ya maafa, hatua iliyochangia kupunguza athari za kifedha walizokumbana nazo na kurejesha utulivu katika utendaji wao wa kazi; na
viii. Kuratibu uwekezaji (SUKUK) umefanyika kwa mafanikio, ambapo malipo ya awali ya faida ya uwekezaji yamelipwa kwa wawekezaji 412 pamoja na taasisi 3 kwa wakati. Hatua hii imeimarisha imani ya wawekezaji na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa uwekezaji wa Serikali.

**PF0502 – Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**33. Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya Ofisi na progamu hii imejumuisha programu ndogo (3) ambazo ni programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja, program ndogo ya Utawala na Uendeshaji Pemba na programu ndogo ya Uratibu wa Mipango na Sera. Hadi kufika Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 9.652 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 11.178 bilioni** katika kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha uwezo wa watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya kitaaluma na mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali, hatua iliyochangia kuongeza ufanisi na weledi kazini. Aidha, wafanyakazi 15 wamewezeshwa kulipiwa mitihani ya CPA;
ii. Uandaaji wa Mpango Endelevu wa Biashara (Business Continuity Plan) unaendelea na kufikia asilimia 75 ya utekelezaji, huku hatua zilizobaki zikiendelea kukamilishwa;
iii. Kuandaa taarifa za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kukamilisha uandaaji wa mpango Mkakati wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za ofisi; na
iv. Wafanyakazi wawili (2) walihudhuria mafunzo ya Uandaaji wa Mpango wa kudhibiti Vihatarishi pamoja na mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini.

**Fungu F06 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

**34. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F06 limepangiwa kutumia **TZS 6.479 bilioni.** Katika kipindi cha Julai – Machi 2026, fungu hili limetumia **TZS 3.808 bilioni** sawa

na asilimia 76 ya makadirio ya **TZS 5.038 bilioni** ya kipindi cha tathmini Matumizi hayo yamejumuisha Programu kuu mbili ambazo ni: -

**PF0601- Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini**

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalengo la kuboresha ukaguzi wa ndani unaozingatia vihatarishi ili kuhakikisha utambuzi, tathmini, na usimamizi madhubuti wa vihatarishi program hii imejumuisha programu ndogo tatu (3) ambazo ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Kamati za Ukaguzi na Taarifa Jumuishi za Ukaguzi wa Ndani, Programu ndogo ya Usimamizi wa Uthibitisho wa Ubora na Programu ndogo ya Uchunguzi wa Ubadhirifu na Vihatarishi hadi kufikia Machi 2026, Programu imetumia **TZS 0.256 bilioni** sawa na asilimia **26** ya makadirio ya **TZS 0.991 bilion**i ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zikiwemo:-

i. Ofisi imefanikiwa kuandaa miongozo mbali mbali ya ukaguzi ikiwemo Muongozo wa taratibu za ukaguzi unaozingatia Viashiria Hatarishi ***(risk-based audit procedural manual)***, Muongozo wa Ukaguzi wa Ndani ***(Internal Audit guideline)*** na Muongozo wa Ukaguzi wa TEHAMA. Miongozo hiyo inatarajiwa kuweka mfumo wa kitaalamu na wa kimkakati utakaowawezesha wakaguzi wa ndani kupanga, kutekeleza na kuripoti kazi za ukaguzi kwa kuzingatia maeneo yenye viashiria hatarishi, ili kuimarisha ufanisi katika Taasisi za Serikali;

ii. Kusomesha jumla ya wakaguzi **75** katika mafunzo ya kitaalamu katika (Proffessional certification) za CIA (23), CISA (37), CFE (3) na CPA (12) ikiwa na lengo la kuboresha kada ya Ukaguzi wa ndani;

iii. Kufanya Kaguzi Maalum katika Taasisi tano za Serikali ambazo ni Baraza la Manispaa Kaskazini A, Hospitali ya Mnazi Mmoja,

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani na Wakala wa Barabara. Kaguzi hizi zimefanyika kwa lengo la kufanya uchanganuzi na utambuzi wa mapato na matumizi, manunuzi na mikataba, TEHAMA pamoja na ufuataji wa Sheria na Miongozo (Compliance);

iv. Kutayarisha Ripoti Jumuishi ya Ukaguzi wa ndani inayojumuisha Taasisi zote za Umma. Ripoti hii inalengo la kutoa tathmini ya pamoja kuhusu hali ya mifumo ya udhibiti wa Ndani, usimamizi wa Viashiria hatarishi pamoja na utawala bora ili kuboresha uwajibikaji na ufanisi wa Taasisi hizo katika kutoa huduma kwa Jamii;

v. Kutoa mafunzo mbali mbali yakiwemo mafunzo juu ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Ndani (Global Internal Audit Standard), mafunzo ya Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini (BAMAS), Mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Ukaguzi, mafunzo yanayohusiana na ukaguzi wa Miradi, Manunuzi na Mikataba. Mafunzo haya yalifanyika kwa wakaguzi wa ndani Unguja na Pemba ambayo yalikuwa na lengo la kujenga na kuimarisha uwezo wa wakaguzi wa ndani Serikalini; na

vi. Kufanya uhakiki wa ubora (Quality Assurance) na ufuatiliaji wa kazi za Wakaguzi wa Ndani katika Taasisi 12 za Umma zikiwemo Mkoa wa Kusini Unguja, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Baraza la Mji Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Baraza la Wawakilishi, Baraza la Mji Kaskazini B, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Pemba, Baraza la Manispaa Chake Chake na Baraza la Mji Micheweni.

**PF0602 - Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala**

**36. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalengo la kuimarisha mifumo ya utawala wa taasisi, kukuza uwezo wa watumishi na kuboresha ubora pamoja na ufanisi. Programu hii imejumuisha programu

ndogo mbili (2) ambazo ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imetumia **TZS 3.551 bilioni** sawa na asilimia 88 ya makadirio ya **TZS 4.048 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zikiwemo:-

i. Kutayarisha Mpango Mkakati ambao umeainisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2025/2026-2029/2030);
ii. Kuandaa muongozo wa 'Enterprise Architecture' ili kutoa ramani inayoonesha uhusiano kati ya mikakati ya kazi za Ofisi na mifumo ya TEHAMA. Kupitia muongozo huu, Ofisi itaweza kuondoa urudufu (duplication) wa mifumo na taarifa, kuimarisha ubora wa taarifa, na kuhakikisha kuwa uwekezaji wa teknolojia unaelekezwa moja kwa moja katika kuimarisha ufanisi wa ukaguzi na ufuatiliaji wa rasilimali za umma;
iii. Kuratibu ushiriki wa wakaguzi wa ndani katika makongamano yanayoandaliwa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Tanzania ili kujadili mafanikio, changamoto na muelekeo wa ukaguzi wa ndani katika kusaidia kufanikisha malengo ya Dira 2020-2050; na
iv. Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watendaji wa Ofisi ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

**Fungu F07 Ofisi ya Msajili wa Hazina**

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu F07 limepangiwa kutumia **TZS 7.609 bilioni**. Katika kipindi cha Julai – Machi 2026, fungu hili limetumia **TZS 4.520 bilioni** sawa na asilimia **77** ya makadirio ya **TZS 5.856 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Matumizi hayo yamejumuisha Programu kuu mbili (2) ambazo ni:-

**PF0701 Programu Kuu ya Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma**

38. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2026, programu imetumia **TZS 2.823 bilion**i sawa na asilimia 98 ya makadirio ya **TZS 2.886 bilioni** ya kipindi cha tathmini Programu hii imejumuisha programu ndogo mbili (2) ambazo ni programu ndogo ya Usimamizi wa Mali za Umma na program ndogo ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma na kutekeleza shughuli zikiwemo:-

i. Kuandaa miongozo mitano (5) kwa ajili ya kuboresha na kurahisisha usimamizi wa Mashirika ya Umma. Miongozo hiyo ni Muongozo wa Uandaaji wa Sera ya Gawio, Muongozo wa Uandaaji wa Mapendekezo ya Miundo kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma, Muongozo wa Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mishahara na Maslahi, Muongozo wa Tathmini ya Bodi, pamoja na Muongozo wa Uandaaji wa Bajeti kwa Mashirika ya Umma;

ii. Kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa PBZ ambapo gawio la TZS 10 bilioni lilitangazwa na kusaini mikataba minne (4) ya makubaliano ya ulipaji gawio;

iii. Kusainiwa kwa mikataba ya kiutendaji na Wenyeviti wa Bodi za Mashirika ya Umma 11 kwa mwaka 2025/2026, pamoja na kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa Mashirika ya Umma 12 kwa mwaka 2024/2025. Hatua hii inalenga kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa utendaji;

iv. Kuandaa nyenzo ya ufuatiliaji (Monitoring Tool) pamoja na nyenzo ya tathmini ya Mkataba wa Utendaji Kazi (Performance Contract Evaluation Tool). Nyenzo hizi zitasaidia kuingiza taarifa za mashirika, ili kutathmini utendaji na kubaini mafanikio au changamoto za mashirika;

v. Kufanya uchambuzi wa bajeti kwa mashirika sita (6) ya uwekezaji wa umma ambayo ni PBZ, ZIC, ZSTC, ZHC, SHIPCO na ZPC kwa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi yaliyowekwa, kwa lengo la kukadiria kiwango cha gawio na kutathmini hali halisi ya utekelezaji wa shughuli zao;
vi. Kuendelea kusimamia uondoaji wa mali chakavu pamoja na ukodishwaji wa mali za Serikali katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, ambapo taasisi **52** zilifikiwa. Aidha ilisimamia uthamini na ukodishaji wa mali mbalimbali za Serikali ikiwemo mashamba, bohari na majengo; na
vii. Kutoa uelewa wa Sera na Mkakati wa usimamizi wa mali za umma kwa Taasisi za serikali (Unguja na Pemba) katika hatua ya awali, na kuendelea na mafunzo kwa taasisi 120 katika hatua ya pili ili kuwezesha uingizaji wa taarifa kwenye mfumo. Hadi sasa, jumla ya mali 4,464 zenye thamani ya TZS 660.376 bilioni zimeingizwa kwenye mfumo.

**PF0702 Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili Hazina**

39. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2026, programu hii imetumia **TZS 1.697 bilioni** sawa na asilimia **57** ya makadirio ya **TZS 2.969** bilioni ya kipindi cha tathmini. Programu hii imejumuisha programu ndogo mbili (2) ambazo ni programu ndogo Usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na program ndogo ya Uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Pemba. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuwalipia ada ya masomo ya muda mrefu watumishi wawili (2) Pamoja na kuwalipia ada ya mafunzo ya muda mfupi ya ICT watumishi kumi na tano (15) sambamba na malipo ya mtumishi mmoja aliyepata mafunzo ya Ukutubi;

ii. Ofisi ya Msajili wa Hazina – Pemba ilisimamia kwa mafanikio ulipaji wa mishahara, posho za wafanyakazi na malipo kwa wazabuni wa huduma na bidhaa mbalimbali, pamoja na kusimamia uingizaji wa taarifa za mishahara kwa watumishi 12 kwenye mfumo wa payroll ambao tayari wameanza kupokea mishahara kupitia mfumo huo;
iii. Kuandaa mafunzo ya uchambuzi wa taarifa kwa kuwashirikisha maafisa wa Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza uelewa wa matumizi ya Microsoft Excel (Advanced), kuboresha uingizaji na usafishaji wa taarifa pamoja na kuimarisha uchambuzi na uandaaji wa ripoti;
iv. Kuendelea na ziara ya kukagua vyombo vya moto kwa Taasisi/ Wizara 13 na kufanikiwa kubaini uwepo wa vyombo vya moto chakavu ambapo Ofisi iliomba utaratibu wa kufanya uondoaji wa vyombo hivyo ufanyike mara moja; na
v. Kufanya ziara ya kutembelea Mashamba 4 yanayomilikiwa na Wizara ya Kilimo katika maeneo mbali mbali kama vile Wesha, Weni na Tumbe. Lengo la ziara hiyo ni kuyatambua mashamba hayo, hali halisi na maeneo yalipo kwa lengo la kufanya makabidhiano ya moja kwa moja kutoka katika umiliki wa Wizara ya Kilimo kuja katika umiliki wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa matumizi kwa mafungu unaonekana katika **kiambatanisho namba 2**.

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

40. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imelenga kutekeleza programu tano (5) na Miradi saba (7) ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, imetumia

TZS 517.981 bilioni sawa asilimia 73 ya makadirio ya **TZS 707.017 bilioni** kwa mwaka. Fedha hizo zimejumuisha fedha za ulipaji wa fidia **TZS 119.627** na Ulipaji wa madeni **TZS 304.69**. Fedha hizi zimetumika kutekeleza Programu na Miradi ifuatayo:-

**Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali.**

41. **Mheshimiwa Spika,** Program hii ina lengo la kuboresha mazingira ya kazi, kuongeza ufanisi na utoaji huduma bora. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Programu imetumia **TZS 67.992 bilioni** sawa na asilimia **54** ya makadirio ya **TZS 126.298** bilioni kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Kuendeleza ujenzi wa Taasisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Shirika la Magazeti - Tunguu, Ofisi ya Nyaraka – Kilimani, Chuo cha Utawala wa Umma - Pujini Pemba; na

ii. Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali na Baraza la Wawakilishi katika eneo la Kisakasaka.

**Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG - Z)**

42. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu, haiba ya Zanzibar na kukuza maendeleo ya kiuchumi katika utoaji wa huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Programu imetumia **TZS 5.521 bilioni** sawa na asilimia **17** ya makadirio ya **TZS 32.5 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Kukamilisha michoro ya mradi wa Utalii katika Kijiji cha Nungwi, Chwaka na Makunduchi pamoja na Mradi Salama wa Watembea kwa Miguu katika Mji Mkongwe (Unguja);

ii. Kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi wa vizimba vya kukusanyia taka na vituo vya kusafirishia taka ngumu pamoja na Kulipa fidia kwa waathirika wa mradi wa Ujenzi wa Vituo hivyo; na
iii. Kuwajengea uwezo maafisa 116 katika maeneo tofauti yakiwemo usimamizi wa kodi ya ongezeko la thamani na uchambuzi wa misamaha ya kodi na mafunzo ya usimamizi wa fedha na "Data Cadastral".

## Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP-VI)

**43. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuimarisha mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu imetumia **TZS 2.089 bilioni** sawa na asilimia **44** ya makadirio ya **TZS 4.75 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Kufanya mapitio ya Sheria, Sera na Kanuni zinazohusiana na mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi ikiwemo sera ya gawio ambayo imekamilika;
ii. Kuandaa utafiti wa mtazamo wa utumiaji wa mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki matokeo ya awali yanaonesha bado kuna tatizo la uwelewa kwa watumiaji wa mfumo huo;
iii. Kuwajengea uwezo maafisa katika masuala ya mageuzi ya fedha za umma kupitia mafunzo maalum katika fani mbalimbali, ikiwemo kodi, manunuzi na usimamizi wa miradi; na
iv. Kuandaa hadidu rejea ya tathmini ya Uwajibikaji na Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (Public Expenditure Financial Accountability) ambapo kwa sasa hatua za kumtafuta mshauri elekezi zinaendelea.

**Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)**

44. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la mradi huu ni kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mradi umetumia **TZS 0.05 bilioni** sawa na asilimia **100** ya makadirio ya **TZS 0.05 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo kufanya mikutano ya Wadau kuhusu Sheria ya mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi na kuandaa Sheria ya Madini kwa upande wa Zanzibar.

**Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar**

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuwainua wananchi kiuchumi kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Programu imetumia **TZS 1.92 bilioni** sawa na asilimia **43** ya makadirio ya **TZS 4.5 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo: -

    i. Kuratibu uandaaji wa mikutano minne (4) ya uhamasishaji wananchi kushiriki katika zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi na utoaji wa hati, ambapo jumla ya hati 555 Unguja na 236 kwa Pemba zimetolewa kwa wananchi. Aidha vikao viwili vya wataalamu vimefanyika kujadili utekelezaji wa shughuli za Programu. Vile vile ziara tatu za ufuatiliaji wa shughuli za Programu zimefanyika Unguja na Pemba kwa kutembelea maeneo yaliyopimwa katika maeneo ya Maungani, Nganani – Makunduchi kwa upande wa Unguja na Makangale na Mfikiwa kwa upande wa Pemba Pamoja na kutembelea vituo vya Masjala ya Ardhi Makunduchi, Mwanakwerekwe na Masjala ya Biashara katika ofisi za BPRA Unguja;

ii. Kuratibu ununuzi na ufungaji wa Makabati ya kielektroniki ya uhifadhi wa taarifa za Ardhi na Biashara katika kituo cha Masjala ya Ardhi Makunduchi na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) Zanzibar na ununuzi wa vitendea kazi mbali mbali ikiwemo Kompyuta, printa na vyombo vya maringi mawili kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji na ufuatiliaji kwa shughuli za program; na
iii. Kuratibu ziara ya kimafunzo kwa watendaji tisa jijini Dodoma kwa ajili ya kupata uelewa wa namna ya kufanya shughuli za upimaji na usajili wa Ardhi kwa kutumia mashirikiano kati ya serikali na mashirika binafsi kwa lengo la kujuwa mbinu mbali mbali zinazoweza kutumika ili kurahisisha shughuli za upimaji na usajili wa Ardhi kwa muda mfupi. Aidha watendaji nane (08) wamepatiwa mafunzo katika Ofisi za Mrajisi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam ambapo wameweza kujifunza kwa vitendo mbinu bora za usajili wa Ardhi iliyowekwa rehani (Mortagage).

**Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo**

46. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuratibu shughuli za upangaji na usimamizi wa rasilimali fedha zinazotengwa na kutolewa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Programu imetumia **TZS 9.551 bilioni** sawa na asilimia **174** ya makadirio ya **TZS 5.5 bilioni** kwa mwaka. Ongezeko hilo limetokana na masuala ya uthamini wa fidia katika miradi ya maendeleo na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Kuratibu vikao vinne (4) vya Kamati ya Uongozi pamoja na vikao 14 vya Kamati Saidizi kwa lengo la kufanikisha mashindano ya CHAN kwa ufanisi mkubwa wa kuiweka tayari Zanzibar kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027 yatakayofanyika kwa pamoja Kenya, Uganda na Tanzania. Aidha, mashindano hayo yalifanyika kwa ufanisi na sasa Serikali inaendelea na matayarisho

ya AFCON;

ii. Kupokea Ripoti 195 zilizoidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali za uthamini wa Mali na vipando vya wananchi walioathirika kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Miongoni mwa miradi hiyo ni kutoka katika Sekta ya Afya, Ujenzi na Uchukuzi, Maji, Nishati na Madini, kilimo, Uchumi wa buluu na Uvuvi;

iii. Kuandaa muongozo wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa program ya miradi ya maendeleo na kufanya mapitio ya muongozo wa uandaaji wa program/Miradi ya maendeleo pamoja na Muongozo wa uandaaji wa mipango Mikakati (SP). Aidha, vikao kazi vya kupitia rasimu za miongozo hiyo vimefanyika kwa watendaji mbali mbali wa Serikali kwa lengo la kupata maoni na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha na kuwa na miongozo itakayotekelezeka; na

iv. Kuratibu uandaaji wa Rasimu ya awali ya Mpango wa Maendeleo wa muda wa Kati (ZADEP II 2026-2031) ambapo kwa sasa rasimu hiyo inatumika katika kukusanya maoni na michango itakayosaidia kuboresha uandishi wa Mpango huo. Zoezi la ukusanyaji maoni linaendelea kwa wadau mbali mbali Unguja na Pemba;

v. Kuandaa Mfumo Jumuishi wa Uratibu wa Mipango ya Maendeleo (ZiPS) kwa MDAs na LGAs na unaendelea katika hatua ya uingizaji taarifa za Programu/Miradi inayotekelezwa kupitia Wizara na Taasisi za Serikali.

**Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Maendeleo (ZADEP, ZDV 2050, SDGs na African Agenda)**

47. **Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini kwa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango

wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Programu imetumia **TZS 1.009 bilioni** sawa na asilimia **56** ya makadirio ya **TZS 1.8 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zikiwemo:

i. Ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2024) imeandaliwa na kuunganishwa na ripoti ya Tanzania Bara kupata ripoti ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo iliwasilishwa New York Marekani katika Jukwaa la Juu la siasa la Umoja wa Mataifa;
ii. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar (ZADEP 2021-26 - End Term Evaluation), Kazi hii inaendelea kwa sasa ipo katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa na ikikamilika itaonesha hali halisi ya utekelezaji wa Mpango kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050;
iii. Tathmini zimefanyika kwa miradi 2 sawa na asilimia 40 kati ya miradi 5 iliyopangwa ambayo ni Mradi wa kiwanda cha kusarifu dagaa na Ujenzi na ukarabati wa maghala;
iv. Jumla ya maafisa ufuatiliaji na tathmini na maafisa mipango 150 kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa Unguja na Pemba wamejengewa uwezo juu ya dhana ya ufuatiliaji na tathmini. Mafunzo haya yatawezesha maofisa hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
v. Maafisa 4 walishiriki katika Kongamano la Wiki ya Ufuatiliaji na Tathmini jijini Mwanza, ili kuimarisha uelewa na ujuzi wa kitaalam katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini, kubadilishana uzoefu na mbinu bora, na kuimarisha mtandao wa ushirikiano na wadau mbalimbali.

**Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati Zanzibar**

48. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuimarisha tafiti na bunifu ili ziweze kusaidia katika mipango, uchumi na maendeleo kwa kufanya maamuzi sahihi na yenye ushahidi. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mradi umetumia TZS 0.481 bilioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya TZS 1.0 bilioni kwa mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuandaa muongozo wa Tafiti za Kitaifa (Research and innovation Grant Manual) ambapo kwa sasa hatua za uchapishaji zinaendelea;
ii. Kufanya Tathmini ya utekelezaji wa Ajenda ya Utafiti ya 2021-2026 na matokeo yake kutumika katika kuandaa Ajenda mpya ya utafiti 2026-2031;
iii. Kukamilisha utafiti wa Kimkakati wa kuliendeleza Zao la Karafuu na Kuandaliwa kwa Programu ya Maendeleo ya Karafuu. Programu hiyo inatarajiwa kusaidia kuongeza uzalishaji wa karafuu na kuimarisha uongezaji wa thamani na masoko pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi. Aidha, Maandalizi ya uandaaji wa Mkakati wa kuendeleza zao la chumvi Zanzibar yanaendelea; na
iv. Kuratibu kikao cha uandaaji wa Muelekeo wa Ubunifu wa Zanzibar ambapo wadau 45 walishirikishwa kutoka sekta mbali mbali.

**Mradi wa Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu IPSAS Accrual**

49. **Mheshimiwa Spika,** lengo la mradi huu ni kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma kupitia mfumo wa IPSAS Accrual ambao utatoa taswira kamili ya hali ya kifedha ya nchi. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mradi umetumia **TZS 0.075 bilioni** ya makadio ya **TZS 1.023 bilioni** kwa mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutoa mafunzo ya awali kwa

wahasibu, maafisa ununuzi na watunza ghala, kuandaa miongozo na "Templates" ambayo imetumika kuandaa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na kuboresha moduli ya ununuzi (Purchase Module), kujifunza namna ya uingizaji wa taarifa za awali (Opening Balance) na kufanya marekebisho (adjustment) ya hesabu za mwisho wa mwaka kazi ambayo imefanywa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Tanzania Bara na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

**Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II)**

**50. Mheshimiwa Spika,** Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) lengo lake ni kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar ili kuwezesha upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mradi umetumia **TZS 4.086 bilioni** sawa na asilimia **89** ya makadirio ya **TZS 4.598 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha zoezi la ukusanyaji wa Taarifa za Utafiti uwandani na kazi inayoendelea kunatengeneza majadueli na uhakiki wa taarifa kabla ya kuanza kwa kazi ya uandishi wa ripoti;
ii. Kufanya uchambuzi wa taarifa za vijijini ambapo kwa Unguja vijiji viliotumika ni Mkokotoni, Kinyasini, Chwaka na Dunga na kwa upande wa Pemba ni soko la mkoani, kiungoni, mtambile na konde. Taarifa zilizokusanywa ni za kipindi cha mwaka mzima (Rural Sensitivity Analysis) na matokeo yanaonesha kuwa kutokusanya taarifa za vijijini hakuna athari katika mfumko wa bei wa Zanzibar;
iii. Kukamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya HBS - Tanzania 2025 na hadi kufikia Machi

2026 Rasimu ya ripoti ya viashiria muhimu ambavyo si vya umasikini (Non monitoring poverty) (elimu, afya, makazi, maji na mazingira) imekamilika;

iv. Kukamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2024/2025 kwa sasa hatua iliyokuwepo ni kufanya uhakiki wa taarifa za ILFS 2025 ambapo ripoti inatarajiwa kutoka mwezi Juni 2026; na

v. Kukamilisha ripoti ya utekelezaji wa zoezi la sensa (methodological report) na kuonesha changamoto zilizojitokeza zitaweza kutatuliwa kwa sensa zijazo. Aidha ripoti imefanyiwa mapitio na timu ya wataalamu kutoka EAC na kuwasilisha mapendekezo hayo kwa NBS/OCGS mwezi wa Machi 2026, kwa ajili ya mapitio ya ripoti hiyo.

**Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia**

51. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la mradi huu ni Kuimarisha uzalishaji na matumizi ya takwimu za jinsia ambazo husaidia katika kubuni sera na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambayo inazingatia mahitaji na haki za kila jinsia. Katika Kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mradi huu umetumia **TZS 0.799 bilioni** sawa na asilimia **34** ya makadirio **TZS 2.32 bilioni** kwa mwaka na kutekeleza wa shughuli zikiwemo:-

i. Kukamilisha uandaaji wa nyenzo za Utafiti wa afya ya wanawake na uzoefu katika maisha (VAW). Aidha, nyenzo hizo zimekamilika na majaribio ya awali yamefanyika katika shehia ya Dimani katika maeneo mawili (2) Ndambani na Chomoani Pamoja na kutoa matoleo matatu (9) ya udhalilishaji na kusambazwa kwa wadau kwa njia ya Tovuti, machapisho na Vyombo vya Habari;

ii. Kufanya kongamano la wadau wa takwimu kutoka taasisi za serikali na binafsi kwa lengo la kuhamisha matumizi ya Takwimu ambapo jumla ya wadau 100 walishiriki kongamano hilo; na
iii. Kutoa mafunzo ya uratibu wa takwimu za jinsia wa taasisi za serikali kwa ajili ya Kutoa uelewa juu ya umuhimu wa Taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** fedha za miradi hiyo zinaonekana katika **kiambatanisho namba 3**

## F. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

### *Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)*

### Mapato

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imekusanya **TZS 826.974 bilioni** sawa na asilimia **94** ya makadirio ya **TZS 878.579 bilioni** katika kipindi cha tathmini. Ufanisi huu umetokana na sababu mbalimbali zikiwemo:

i. Uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Kuimarika kwa uhiari wa ulipaji kodi kumechochewa na juhudi za elimu kwa walipakodi kupitia kampeni ya "ZRA Mtaani Kwako," ambazo zimeongeza uelewa na kuimarisha uwajibikaji wa ulipaji kodi. Sambamba na hilo, kumekuwa na ongezeko la idadi ya watalii nchini pamoja na usajili wa walipakodi wapya;

iii. Kuwepo kwa Matokeo chanya yanayotokana na Zoezi la kuunganisha Mifumo kati ya Mifumo ya Walipakodi na Mifumo ya ZRA hasa katika biashara ya Hoteli za Kitalii;
iv. Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) sambamba na kuimarika kwa Mahusiano na Ushirikiano kati ya ZRA, Wafanyabiashara na wadau wengine kulikopelekea kuongezeka kwa ulipaji kodi wa hiari; na
v. Kuimarika kwa uwajibikaji na weledi wa watumishi wa ZRA kumechangia kuimarika kwa uthabiti katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato.

**Matumizi**

**53. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mamlaka ya Mapato Zanzibar imetumia **TZS 23.480 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya **TZS 24.04 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Kati ya fedha hizo **TZS 21.547 bilioni** zilitumika kwa kazi za kawaida na **TZS 1.940 bilioni** zilitumia kwa kazi za Maendeleo na kufanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. ZRA inaendelea na utaratibu wa kuwafikia na kuwasajili walipakodi waliopo nje ya Zanzibar wanaojishughulisha na utoaji wa huduma za kibiashara katika jukwaa la kimtandao Jumla ya walipakodi saba (7) wamesajiliwa na ZRA kutokana na huduma za biashara ya mtandao aidha, jumla ya **TZS 3,293,947,337.25** zilikusanywa kwa lengo Kukusanya kodi katika huduma za kidijitali (Digital Service Tax);
ii. ZRA imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika uchunguzi wa mifumo ya kifedha (Forensic Tools) ambapo Mamlaka imefanikiwa kupata na kusimika programu mbili za uchunguzi, ambazo ni OS Forensic na Oxygen Forensic, ambazo

zinaendelea kutumika katika kufuatilia na kuchambua taarifa za mifumo ya kifedha. Aidha, ZRA inaendelea na mchakato wa kuhuisha na kuboresha programu hizo ili kuongeza ufanisi na usahihi katika uchunguzi wa masuala ya kifedha; na

iii. ZRA katika kutekeleza majukumu yake imefanya mikutano kumi na mbili (12) katika Mikoa ya Kikodi ya Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa ufafanuzi kuhusu mabadiliko ya sheria mbali mbali za kodi yaliyofanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026. Hatua hii imesaidia kuongeza uelewa wa wadau na kuimarisha utekelezaji wa sheria za kodi kwa ufanisi zaidi.

***Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)***

54. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar imefanikiwa kukusanya **TZS 616.505 bilioni** sawa na asilimia **102** ya makadirio ya **TZS 605.773 bilion**i kwa kipindi cha tathmini. Mafanikio hayo yanatokana na mikakati iliyotekelezwa ikiwemo: -

i. Kuanzisha kwa mfumo wa pamoja wa uondoshaji wa shehena maeneo ya Forodhani (Tanzania Electronic Window System) ulio saidia kuharakisha uondoshaji wa shehena bandarini; na

ii. Kuunganisha mifumo na baadhi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kutoa elimu na mafunzo ya kodi kuhusu mabadiliko ya sheria mbalimbali kwa wananchi.

***Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)***

55. **Mheshimiwa Spika,** Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, ilitarajia kupata Mapato kutoka vyanzo vyake vya riba na visivyo na riba **TZS 223 bilioni** na ikafanikiwa kupata mapato halisi **TZS 201 billioni** ambayo ni sawa na asilimia **90** ya lengo. Mapato hayo sawa na ongezeko la asilimia **24** ya

mapato ya **TZS 162 bilioni** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2025 hii imetokana na Uboreshaji wa mikakati ya uuzaji wa huduma za kifedha, Upanuzi wa mtandao wa matawi na huduma bora.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Benki imetumia **TZS 111 bilioni** ni sawa na asilimia 90 ya lengo ukilinganisha na matarajio ya matumizi ya **TZS 124 bilioni**. Matumizi haya yametokana na shughuli za uendeshaji wa Benki, uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA, pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma.

57. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi Julai hadi Machi 2026, Benki imefanikiwa kupata Faida **TZS 90.0 bilioni** ukilinganisha na kiwango kilichokadiriwa cha **TZS 100 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia 90 ya lengo. Faida hiyo sawa na ongezeko la asilimia 24 ya **TZS 73 billioni** zilizopatikana kwa mwaka 2025. Hili limetokana na ufanisi katika usimamizi wa mikopo mikubwa ya kibiashara iliyotolewa kwa wateja wa sekta mbalimbali, kupanuka kwa huduma za kifedha, pamoja na kudhibiti gharama na ongezeko la mapato kutoka kwa shughuli za biashara.

58. **Mheshimiwa Spika,** rasilimali za Benki zilifikia **TZS 3.0 trilioni** hadi Machi 2026, ikilinganishwa na lengo la **TZS 3.4 trilioni** kwa mwaka 2026 na kuifanya PBZ kuendelea kuwepo kwenye orodha ya mabenki makubwa nchini Tanzania. Ukilinganisha na kipindi kama hicho cha mwaka 2025 rasilimali za benki zilikua **TZS 2.6 trillion** ikiwa sawa ongezeka la asilimia **15.** Hii imetokana na ongezeko la mikopo inayotolewa kwa wateja, pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa mali na rasilimali za benki.

59. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Amana za wateja (deposits) zilifikia **TZS 2.5 trilioni** ambayo ni sawa na asilimia 86 ya mafanikio ukilinganisha na amana ya **TZS 2.7 bilioni** tuliyokadiria kupata kwa mwaka 2026. Ufanisi huu unatokana na kuimarika kwa uhusiano na wateja, mikakati bora ya uhamasishaji wa amana, pamoja na kuongezeka kwa imani ya wateja katika huduma za Benki.

60. **Mheshimiwa Spika,** Mtaji wa benki hadi kufikia Machi 2026 umefikia **TZS 333 bilioni**, sawa na ongezeko la asilimia **27** ya mtaji wa **TZS 262 bilioni** kwa mwaka 2025. Ongezeko hili limetokana na ukuaji wa biashara, ufanisi katika usimamizi wa rasilimali, pamoja na juhudi za kuongeza wateja wapya na kuboresha huduma za kifedha ambazo zimesababisha kuongezeka kwa mapato na kuimarika kwa mtaji.

61. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, mikopo kutoka katika sekta tofauti imefikia **TZS 1.66 trilioni** sawa na asilimia 84 ya makadirio ya **TZS 1.96 trilioni** kwa mwaka wa fedha 2026. Mafanikio haya yametokana na uboreshaji wa mazingira ya kifedha, ikiwemo utekelezaji wa sera rafiki za mikopo.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Benki imefanikiwa kulipa kodi kwa TRA na ZRA ya **TZS 47.6 bilioni** ukilinganisha na kiwango cha **TZS 34 billioni** kilicholipwa katika kipindi kama hicho cha 2025. Aidha, Benki imefanikiwa kukamilisha ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka 2025 na kupata matokeo chanya, ambapo ilihitimisha mwaka kwa faida ya **TZS bilioni 110**, mafanikio haya yatawezesha benki kutoa gawio kwa Serikali.

**MIRADI**

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi, iliyofanikiwa ndani ya kipindi cha Julai mpaka Machi 2026 ni pamoja na:-

   i. Kuanza kwa utoaji wa huduma za kibenki kituo cha Ubungo, pamoja na kuboresha tawi la Mpirani kuwa katika muonekano wa kisasa;
   ii. Kuanza kwa utoaji wa huduma za kibenki tawi la Arusha, pamoja na vituo vya kutolea huduma vya Konde na Madungu kwa upande wa pemba;
   iii. Kufanikiwa kuwa na mawakala 2,311 ukilinganisha na kipindi kama hicho cha mwaka 2025 ilikua na mawakala 1,626 ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 42;
   iv. Benki imefanikiwa kuongeza ATM 3 na kufanya PBZ kufikia idadi ya ATM 55;
   v. Benki imefanikiwa kuanzisha huduma ya LIPA HAPA, ambayo inawezesha ufanyikaji wa malipo wa huduma na bidhaa kupitia mabenki mengine na mitandao tofauti ya simu kwa uharaka na ufanisi; na
   vi. Kuendelea kuboresha *PBZ App* ili kusaidia wateja kupata huduma iliyokuwa nzuri zaidi na sehemu yoyote na wakati wowote.

***Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA)***

**Mapato**

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/26 Mamlaka ilikadiriwa kukusanya **TZS 1.175 bilioni**. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026 Mamlaka imekusanya **TZS 0.410 bilioni** sawa na asilimia **48** ya makadirio **TZS 0.857 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yametokana na ada ya usajili wa watoa huduma, ada ya nyaraka ya zabuni na ada ya matangazo ya mpango wa ununuzi wa mwaka.

**Matumizi**

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka imepangiwa kutumia **TZS 3.274 bilioni**. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mamlaka imetumia **TZS 1.512 bilioni** sawa na asilimia **62** ya makadirio ya **TZS 2.413 bilioni** ya kipindi cha tathmini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa Taasisi nunuzi kumi na moja (11) na wadau mbalimbali kama wawakilishi, madiwani na wajumbe wa Bodi za Zabuni Unguja na Pemba;
ii. Kufanya mapitio ya nyaraka sanifu za ununuzi nane (8) ambazo ni Kotesheni ya bidhaa, Kotesheni ya kazi, Kotesheni ya huduma isiyo ya kitaalamu, Nyaraka sanifu ya bidhaa kwa ununuzi mkubwa, Nyaraka sanifu ya ushauri wa kitaalamu, Nyaraka sanifu ya mkataba endelevu, Nyaraka sanifu ya kazi za ununuzi mkubwa; na Nyaraka sanifu ya kuandaa na kujenga;
iii. Kukamilisha uandaaji wa fomu na nyaraka za ununuzi wenye thamani ndogo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, ambapo imewezesha upatikanaji wa nyaraka sahihi na kurahisisha mchakato wa ununuzi pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za ofisi;
iv. Kutoa vipindi mbali mbali vya kuitangaza Mamlaka kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC - TV) kwa lengo la kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na Mamlaka, pamoja na kuimarisha taswira na mahusiano na wadau;
v. Kutoa mafunzo ya miongozo ya ununuzi wa umma kwa Taasisi nunuzi 15 za Unguja na Taasisi nunuzi 50 za Pemba, pamoja na kuwajengea uwezo maafisa ununuzi 310 juu ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Mafunzo hayo yamechangia kuimarika kwa uelewa wa taratibu za ununuzi, kuongeza uwazi na uwajibikaji,

pamoja na kuboresha ufanisi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

vi. Kuandaa nyaraka tano (5) sanifu za ununuzi na kutoa mafunzo kwa watoa huduma 164 juu ya matumizi sahihi ya nyaraka hizo. Hatua hii imechangia kuongeza uelewa na ufuataji wa taratibu za ununuzi, kupunguza makosa katika uwasilishaji wa zabuni, pamoja na kuimarisha ushindani wa haki na uwazi katika michakato ya ununuzi wa umma.

***Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)***

66. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima la Zanzibar utekelezaji wa bajeti yake umegawika katika maeneo makuu manne (4), maeneo hayo ni Mapato yatokanayo na mauzo ya bima mbalimbali, bima ya lazima kwa wageni (Inbound Travel Insurance), na mapato yatokanayo na Uwekezaji, matumizi ya uwendeshaji (Management Expenses), matumizi ya Madai kwa wateja na matumizi ya ujira kwa Mawakala na Madalali.

**Mapato**

67. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Shirika limefanikiwa kukusanya **TZS 122.9 bilioni** ya mauzo ya bima ambayo ni sawa na asilimia **112** ya makadirio ya kukusanya **TZS 109.7 bilioni** katika kipindi cha tathmini. Mapato hayo yaliongezeka kwa asilimia 49 ukilinganisha na mapato ya **TZS 82.3 bilioni k**atika kipindi kama hicho cha Julai hadi Machi 2025. Shirika limeweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hayo kwa kipindi hicho kwa kutekeleza mikakati ifuatayo: -

i. Shirika limeendelea kutoa taaluma na kujitangaza kwa Wananchi na kwa Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza mapato ya Shirika;

ii. Shirika limeendelea kuzidisha mashirikiano ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mawakala na madalali wake wanaofanya biashara ya kuuza bima kwa niaba ya Shirika;
iii. Shirika limeendelea kushirikiana kikamilifu na mabenki mbalimbali katika mfumo wa "Bancassurance" kwa lengo la kuongeza mapato yake; na
iv. Shirika limeendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuhakikisha Miradi mikubwa ya Maendeleo na Mkakati kwa Wananchi inakatiwa kinga za bima na Shirika.

**Matumizi**

**68. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Utekelezaji wa matumizi ya Shirika kama ifuatavyo: -

i. **TZS 12.7 bilioni** zilitumika kwa ajili ya gharama za uwendeshaji wa ofisi (Management Expenses) sawa na asilimia **88** ya makadirio ya matumizi katika kipindi cha tathmini ambayo ni **TZS 14.4 bilioni**;
ii. **TZS 8.1 bilioni** zimetumika kulipa madai **884** mbalimbali ya wateja waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima ambayo ni sawa na asilimia 48 ya makadirio **TZS 16.8 bilioni** katika kipindi cha tathmini; na
iii. **TZS 6.26 milioni** zimetumika katika kulipa ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika ambayo sawa na asilimia **64** ya makadirio katika kipindi cha tathmini ya **TZS 9.8 bilioni**.

***Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)***

**Mapato**

**69. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mfuko ulipanga kukusanya mapato ya TZS 281.33 bilioni. Mapato

hayo yalitegemewa kutoka katika vyanzo vikuu viwili, ambapo **TZS 155.08 bilioni** ni michango ya wanachama na **TZS 126.25 bilioni** mapato ya uwekezaji na mapato mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 346.35 bilioni** zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 123 ya ufanisi, ambapo **TZS 135.90 bilion**i kutoka kwa michango ya wanachama na **TZS 210.45 bilioni** kutokana na mapato ya uwekezaji na mapato mengineyo.

**Matumizi**

70. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kutumia **TZS 396.94 bilioni** ikiwa **TZS 83.38 bilioni** kwa ajili ya kulipia mafao, **TZS 299.20 bilioni** kwa ajili ya uwekezaji, **TZS 1.77 bilioni** kwa ajili ya kusimamia miradi na **TZS 12.59 bilioni** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji. Jumla ya **TZS 318.89 bilioni** zilitumika sawa na asilimia **80,** ikiwa TZS 69.18 bilioni kwa ajili ya kulipia mafao, **TZS 239.79 bilioni** kwa ajili ya uwekezaji, **TZS 1.67 bilioni** kwa ajili ya kusimamia miradi na **TZS 8.25 bilioni** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mfuko umesajili waajiri **263** sawa na asilimia **90** ya makisio ya kuwasajili waajiri **293** na hadi sasa Mfuko umekuwa na Waajiri waliosajili wamekifikia **3,668**. Na ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko ulisajili Waajiri **245;**

ii. Mfuko umesajili waajiriwa **12,418** sawa na asilimia **62** ya makisio ya kuwasajili waajiriwa **20,160** na hadi sasa Mfuko umekuwa na Waajiriwa waliosajiliwa wanaofikia **166,464**. Na ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko ulifanikiwa kusajili waajiriwa **11,655;**

iii. Mfuko wa Hiari umesajili wanachama **1,963** sawa na asilimia **24** ya makisio ya kuwasajili wanachama **470.** Hadi sasa idadi

ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wamefikia **13,968** kwa Mfuko wa kujichangia kwa Hiari. Na ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko wa Hiari ulisajili Wanachama 769.

iv. Waajiri **2,505** walitarajiwa kufanyiwa ukaguzi na waajiri **1,070** wamekaguliwa. Na ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025 waajiri **1,767** wamekaguliwa, ikiwa ni ukaguzi wa ufuatiliaji (Follow-up), ukaguzi wa kawaida (Routine) na ukaguzi wa waajiri wapya (Survey Inspection).

v. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mombasa Zanzibar wenye majengo **14** na ujenzi wa Soko la Mombasa imekamilika na utekelezaji kwa asilimia **100.**

vi. Kwa upande wa ujenzi wa kituo cha mabasi Jumbi na Koani, taratibu za kupata eneo la awamu ya kwanza Jumbi limeshakamilika na eneo hilo limeshasafishwa. Kwa upande wa awamu ya pili Jumbi na Koani tayari tathmini imeshakamilika kwa wamiliki wa maeneo hayo na fidia zao zinaendelea kutolewa hadi kukamilika kwake.

***Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)***

**Mapato**

**71. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2026 imeendelea kupokea mapato kutoka kwenye vianzio vyake ambavyo ni Ruzuku na Mapato ya Ndani. Kwa upande wa Ruzuku, ZIAAT imepokea **TZS 1.524 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia **74.7** ya Makadirio ya **TZS 2.039 bilioni**. Kwa upande wa Mapato ya Ndani ZIAAT imekusanya **TZS 0.201 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia **61** ya makadirio ya **TZS 0.328 bilioni**. Mapato hayo yametokana na Ada ya usajili, ada ya mwaka, ada ya Leseni, ada ya mafunzo na ada za mitihani.

**Matumizi**

72. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, imetumia **TZS 1.426 bilioni** sawa na asilimia **70** ya makadirio ya **TZS 2.039 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimejumuisha fedha za mishahara **TZS 0.452 bilioni** na matumizi ya uendeshaji wa Ofisi **TZS 0.974 bilioni**. Ongezeko hili la mshahara limetokana na kuhamishiwa mishahara ya Wafanyakazi waliohamia na kupanda hadhi kwa Taasisi na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. *Kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Resource Mobilization Strategy, Code of Ethics, Risk Management Framework, ICT Policy, Whistleblowing Policy, CPD Guideline, ZFRS 1, Staff Regulations* na mwongozo wa *Field Practical kwa CTT* na *CTP*. Miongozo hii imeimarisha uwazi, uwajibikaji na weledi, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali, kuboresha maadili ya kitaaluma, kupunguza vihatarishi, kuimarisha TEHAMA na kuongeza ujuzi wa vitendo kwa wanafunzi na wahitimu;

ii. Jumla ya wafanyakazi watano (5), wanaume watatu (3) na wanawake wawili (2), wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ili kuimarisha utendaji wa kazi. Aidha, ZIAAT imetoa mafunzo kwa wanachama wake ikiwemo Global Internal Audit Standards (GIAS) kwa wakaguzi wa ndani na mafunzo ya wajumbe wa bodi za taasisi za serikali. Mafunzo haya yamelenga kuimarisha ufanisi wa utendaji, kuongeza uwajibikaji na utawala bora, kuboresha ubora wa ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, pamoja na kuwawezesha wajumbe wa bodi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi zaidi;

iii. Kuanzisha mfumo wa E-Library ili kuwawezesha wanafunzi wa fani za kodi kupata kwa urahisi vitabu, miongozo, sheria na machapisho

ya kitaaluma mtandaoni. Mfumo huu unawasaidia kujisomea wakati wowote na mahali popote, kufanya tafiti na marejeo ya masomo, pamoja na kuongeza uelewa na ujuzi katika taaluma ya kodi; na

iv Kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kitaaluma na kiutendaji kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu bora za uendeshaji na kuimarisha ushirikiano na wadau. Ushiriki huu umeongeza ufanisi wa utendaji, kuboresha maamuzi ya kimkakati na kuendeleza taaluma kwa kuendana na mabadiliko ya kimataifa.

### *Mfuko wa Huduma ya Afya Zanzibar (ZHIF)*

### MAPATO

73. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, umefanikiwa kukusanya **TZS 48.04 bilioni** sawa na asilimia **7**8 ya lengo la kukusanya **TZS 61.43 bilioni.** Aidha ZHSF imepokea **TZS 40.15 bilioni** kutoka Serikalini kwa ajili kufanya malipo kwa kampuni za Uwekezaji (Outsources) zinazotoa huduma za afya kwa hospitali za Serikali za Wilaya na Mkoa.

### Matumizi

74. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Mfuko umefanikiwa kulipa madai ya watoa huduma yenye thamani ya **TZS 12.05 bilion**i huku ukiimarisha udhibiti wa matumizi kupitia mifumo ya kielektroniki ya uhakiki ambayo inasaidia kupitia madai yasiyo na sifa. Aidha Mfuko umelipa **TZS 28.68 bilioni** kwa kampuni za uwekezaji kwa ajili madeni na madai ya wananchi wasiokuwa wanachama wa Mfuko wanaopata huduma katika hospitali za Serikali.

75. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umesajili wanachama **690,335** sawa na asilimia **63** ya lengo la usajili wa **1,089,000**. Kati ya usajili huo

sekta rasmi **51,570,** sekta isiyo rasmi **631,139**, wastaafu **815** na wanafunzi **6,811** na kufanya idadi ya wanachama wote wa Mfuko kuwa **1,015,747** ambayo ni sawa na asilimia 47 ya idadi ya wananchi wa Zanzibar **2,161,086**.

**MAFANIKIO**

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango katika Awamu ya Nane imepata mafanikio yafuatayo: -

i. Kuweza kukusanya kodi zaidi ya asilimia 90 ya kiwango kilichopangwa kwa Taasisi za kodi (TRA na ZRA);

ii. Serikali imeweza kununua gari zaidi ya 150 zinazotumia nishati ya umeme kwa lengo la kupunguza gharama za matumizi ya nishati ya mafuta ambapo gari hamsini (50) tayari zimeshawasili;

iii. Uratibu wa kifedha kwa ajili ya kufanikisha miradi ya kimkakati ikiwemo mradi wa ujenzi wa mji wa serikali pamoja na ujenzi wa Baraza la Wawakilishi;

iv. Wizara imefanikiwa kuongeza huduma za kifedha kwa kutunga Kanuni za Huduma ndogo za Fedha, kufungua matawi, vituo vya huduma, mawakala wa huduma za kibenki na bima pamoja na kuanzisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki;

v. Serikali imefanikiwa kutoa gawio kwa wawekezaji wa Sukuk mia nne na kumi na mbili na taasisi tatu (3) ambapo **TZS 8.641 bilioni** zimetumika.

vi. Kupitia ZSSF, Serikali imetekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zilizopo Mombasa Zanzibar wenye majengo 14 na ujenzi wa Soko la Mombasa, sambamba na ununuzi wa mabasi kumi ya abiria (10) yanayotumia nishati umeme ambayo yameshawasili.

**Changamoto**

77. **Mheshimiwa Spika,** mbali na mafanikio yaliyopatikana Ofisi pia imekumbana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wake ikiwemo: -

i. Kuchelewa kwa baadhi ya taasisi kuwasilisha vielelezo vya kutosha vya Mradi kwa wakati hali unayopelekea kuchelewa kwa mradi kuanza Pamoja na kucheleweshа taratibu na hatua za utekelezaji wa miradi hali inayopelekea miradi hiyo kutekelezwa nje ya muda wa utekelezaji;
ii. Utoaji wa Risiti kwa wafanyabiashara na wananchi kudai risiti bado ni tatizo;
iii. Ufinyu wa eneo la ofisi kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na baadhi ya taasisi zake.
iv. Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) unakabiliwa na shinikizo la kuongezeka kwa gharama kutokana na magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) yanayohitaji matibabu ya gharama kubwa.

**Utatuzi wa changamoto**

78. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imechukua hatua mbali mbali katika kutatua changamoto zilizojitokeza kipindi cha utekelezaji wa majukumu kama ifuatavyo: -

i. Ofisi inaendelea kufuatilia na kusimamia uwasilishwaji wa miradi kwa wakati iliyokidhi vigezo Pamoja na kuboresha usimamizi, ufuatiliaji na utendaji katika utekelezaji wa Miradi sambamba na kusimamia na kuboresha Mfumo wa ZIPs (Zanzibar Intergrated Planning System) kwa lengo kurahisisha upatikanaji wa Taarifa za Miradi tokea awali;
ii. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuwaelimisha wananchi kudai risiti pamoja na kutoa adhabu kwa wafanyabiashara wenye kukiuka suala la utoaji risiti;

iii. Serikali imeanza ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka baada ya mkandarasi na Mbia kupatikana, aidha serikali imelipa malipo yake ya awali kama ilivyo katika mkataba wa makubaliano ya ujenzi huo; na
iv. Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar unatarajia kufanya marekebisho ya kitita chake cha mafao wanayostahiki kupata wanachama wa mfuko.

## G. MAKADIRIO YA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### Vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango

**79. Mheshimiwa Spika,** Bajeti hii imezingatia Dira ya Maendeleo 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo wa muda wa kati ZADEP, Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 - 2030 na Miongozo iliyotolewa katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi. Pamoja na mwenendo wa hali ya uchumi na teknolojia ya mifumo ya kielektroniki katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti upotevu wa mapato, Wizara ya Fedha na Mipango imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali yakiwemo mapato ya ndani na mapato kutoka kwa washirika wa maendeleo;
ii. Kuimarisha Matumizi ya kidijitali katika upangaji na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na kusimamia utekelezaji wa bajeti inayozingatia usawa wa kijinsia;
iii. Kukamilisha Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati ZADEP 2026–2031 pamoja na nyaraka saidizi ikiwemo Mwongozo wa Uandaaji wa Upembuzi Yakinifu na Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango mikakati ya Kisekta na kuratibu utekelezaji wa tafiti za kimkakati Zanzibar;

iv. Kuendeleza na kusimamia ujenzi wa Ofisi, Mji wa Serikali na Baraza za Wawakilishi katika eneo la Kisakasaka;
v. Kuanza ujenzi wa Makao makuu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kuongeza matawi na uwekaji wa mashine za kutolea fedha (ATM);
vi. Kusimamia uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji ZIB (Zanzibar Investment Bank) pamoja na uanzishwaji wa Soko la Hisa la Zanzibar (Zanzibar Stock Market);
vii. Kuandaa na kupitia Sera, Sheria, kanuni na miongozo ya Wizara kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi na kurahisisha utekelezaji wa kazi za Wizara na Serikali. (Kufanya mapitio ya Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) namba 4 ya mwaka 1998 na Kuandaa sheria ya ZSSF na sera ya idadi ya watu) na miongozo ya ununuzi wa vifaa vya TEHAMA pamoja na makundi maalumu;
viii. Kuanzisha, kuimarisha, na kukuza matumizi ya mifumo ya kielektroniki pamoja na kuunganisha mifumo ili iweze kuoana; na
ix. Kuanzisha Bima za Kilimo (Agriculture Insurance) pamoja na Kampuni Tanzu ambayo Inasimamia Bima ya Maisha "ZIC Life Insurance".

**Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Fedha na Mipango**

**80. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Fedha na Mipango inakadiriwa kukusanya **TZS 8,052.83 bilioni** makadirio hayo sawa na ongezeko la asilimia **23** ukilinganishwa na makadirio ya kukusanya **TZS 6,527.59 bilioni** yaliyopangwa kwa mwaka 2025/2026. Ongezeko hili limetokana na kuimarika mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kuimarika kwa mazingira mazuri ya Uwekezaji katika nchi yetu.

81. **Mheshimiwa Spika**, mapato hayo yamekadiriwa kukusanywa katika mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kama ifuatavyo: -

i. Fungu 009 limekadiriwa kukusanya **TZS 7,772.441 bilioni;**
ii. Fungu 022 limekadiriwa kukusanya **TZS 246.277 bilioni**
iii. Fungu 023 limekadiriwa kukusanya **TZS 0.112 bilioni; na**
iv. Fungu 106 limekadiriwa kukusanya **TZS 34 bilioni.**

82. **Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa mapato hayo kwa kila chanzo unaonekana katika **kiambatanisho namba 4**.

**Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango.**

83. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Fedha na Mipango inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 2,078.925** bilioni kwa mafungu saba (7) yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango na uchambuzi wa Mafungu hayo ni kama ifuatavyo: -

i. Fungu 009 imekadiriwa kutumia **TZS 1,322.884 bilioni;**
ii. Fungu 021 imekadiriwa kutumia **TZS 576.693 bilioni**;
iii. Fungu 022 imekadiriwa kutumia **TZS 17.028 bilioni**
iv. Fungu 023 imekadiriwa kutumia **TZS 14.004 bilioni**;
v. Fungu 024 imekadiriwa kutumia **TZS 34.156 bilioni**
vi. Fungu 052 imekadiriwa kutumia **TZS 6.876 bilioni**; na
vii. Fungu 106 imekadiriwa kutumia **TZS 107.284 bilion**i.

84. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa za matumizi naomba kuwasilisha uchambuzi wa matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kila fungu kama ifuatavyo: -

**A.** Matumizi kwa fungu **009** yanakadiriwa kufikia **TZS 1,322.884 bilioni** ambazo zitatumika katika utekelezaji wa programu kuu tatu (3)

85. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo, **TZS 295.852 bilioni** ni mshahara, **TZS 12.445 bilioni** matumizi ya kawaida **TZS 36.861 bilioni** Ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara Fedha na Mipango, na **TZS 977.726 bilioni** fedha za miradi ya maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo:-

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango imekadiriwa **TZS 986.186 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 2.748 bilioni**, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 8.309 bilioni** na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 975.129 bilioni;**

ii. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma imekadiriwa kutumia **TZS 331.554 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara wa watendaji **TZS 1.907 bilioni,** marekebisho ya mshahara (salary adjustment) **TZS 290.646 bilioni,** matumizi za kazi za kawaida **TZS 3.03 bilioni,** fedha za miradi ya maendeleo **TZS 2.597** bilioni, Ruzuku ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar **TZS 30.33 bilioni** na ruzuku ya Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar **TZS 3.042 bilioni**; na

iii. Programu ya Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Huduma za Sheria kifedha imekadiriwa **TZS 5.144 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 0.551 bilioni**, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.105 bilioni** na Ruzuku ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Fedha za Umma **TZS 3.488 bilioni**.

**B.** Matumizi kwa fungu **021** yanakadiriwa kufikia **TZS 576.693 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

86. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo, **TZS 3.522 bilioni** Mshahara, **TZS 573.171 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu Kuu ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali.

**C.** Matumizi kwa fungu **022** Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali yanakadiriwa kufikia **TZS 17.028 bilioni**

**87. Mheshimiwa Spika,** Kati ya Fedha hizo, **TZS 12.689 bilioni** Mshahara, **TZS 0.975 bilioni** Ruzuku inayosimamiwa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, **TZS 3.364 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali **TZS 14.592 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 12.689 bilion**i, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.903 bilioni**; na

ii. Programu ya Usimamizi wa Hazina **TZS 2.436 bilion** fedha hizi zimejumuisha matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.46 bilioni** na Ruzuku ya Kampuni ya Zanzibar Treasury Sukuk 1 Limited **TZS 0.975 bilioni.**

**D.**Matumizi kwa fungu **023** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali **TZS 14.004 bilioni.**

**88. Mheshimiwa Spika,** Kati ya Fedha hizo, **TZS 2.44 bilion**i Mshahara, **TZS 3.047 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS 8.517 bilioni** kwa ajili ya Kazi za Miradi ya Maendeleo.

i. Programu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii imekadiriwa kutumia **TZS 6.994 bilioni** fedha hizi zimejumuisha matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.264 bilioni** na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 5.729 bilioni**; na

ii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali **TZS 7.01 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 2.439 bilioni,** matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.783 bilioni** na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 2.787 bilioni.**

**E.** Matumizi kwa fungu **024** Tume ya Mipango yanakadiriwa kufikia **TZS 34.156 bilioni**.

**89. Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo, **TZS 2.412 bilioni** Mshahara, **TZS 2.724 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 29.02 bilioni** Matumizi ya kazi za Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo:-

i. Programu Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi Programu imekadiriwa **TZS 28.468 bilioni** fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 0.827 bilioni**, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 0.822 bilioni** na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 26.82 bilioni**;

ii. Programu ya Uratibu wa Utafiti na Uchumi Mkuu imekadiriwa kutumia **TZS 3.328 bilion**i fedha hizi zimejumuisha mshahara **TZS 0.464 bilioni**, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 0.664 bilioni** na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 2.2 bilion**i; na

iii. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango imekadiriwa kutumia **TZS 2.36 bilion** fedha hizi zimejumuisha mshahara TZS 1.121 bilioni, matumizi ya kazi za kawaida **TZS 1.239 bilioni.**

**F.** Matumizi kwa fungu **052** Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali yanakadiriwa kufikia **TZS 6.875 bilioni**.

**90. Mheshimiwa Spika,** Kati ya Fedha hizo, **TZS 4.477 bilioni** Mshahara, **TZS 2.398 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

